

Wasiwasi wa Wakimbizi wa Msumbiji:

UHURU WA WARENO HATARI KWA FRELIMO

Ripota wetu, Dar es Salaam, Jumamosi.

"SITAKI kuilaumu Serikali ya Tanganyika," alisema Bw. Camando, na kuongeza, "ila ninasikitishwa na hatua iliyochukuliwa ya kuwaachilia, hatua ambayo naifikiria huenda ikaleta madhara katika chama chetu."

Ili kutaka kuhakikisha juu ya utabiri wake huo, Bw. Camando, alidokeza kuwa, hapo nyuma wakati kulikuwepo vyama viwili vya wakimbizi wa Msumbiji... hapa nchini, alikuja Mzungu mmoja ambaye alidai kwamba alikuja kufungua shule ya kuwasomeshea wakimbizi wa Msumbiji, ili wawe na elimu ya kuweza kuendesha vizuri mambo ya siasa.

Mzungu huyo, kama alivyosema Bw. Camando, alikuwa ni mpelelezi ambaye alitumwa na Serikali ya Kireno.

Akaendelea: "Ushahidi uliotuonyesha ukweli huu ni kule kuchapisha karatasi ambazo alitutaka watu wa Msumbiji sote tulioko Tanganyika, tujiandikishe kwenye karatasi hizo, majina yetu na mahali tulikotoka."

Aliendelea kueleza kuwa Mzungu huyo walikuja kumtambua jinsi alivyokuwa mpelelezi, kwa sababu bakuwambia madhumuni ya kuandikisha majina, yao na makwao kwenye karatasi hizo.

Akamaliza: "... Mzungu huyo, akaendelea, mahali alikokuwa ametoka ni sehemu ile ile ambayo Wareno hawa wawili tuli nao sasa ndiko walikotoka; kwenye sehemu iitwayo Beira na hili ni jambo lenye kututia wasiwasi mwingi."